JORNADA INTERNACIONAL DE LUCHA ANTI-IMPERIALISTA
JOURNÉE INTERNATIONALE DE LUTTE ANTIIMPÉRIALISTE
INTERNATIONAL WEEK OF ANTI-IMPERIALIST STRUGGLE
JORNADA INTERNACIONAL DE LUTAS ANTI-IMPERIALISTA
الأسبوع العالمي للنضال ضد الإمبريالية

Wanawake Wavujajasho Duniani Unganeni Kupambana na Ubeberu katika Siku ya Wanawake Duniani.

**Machi 8, 2021**

Katika Siku ya Wanawake Duniani, sisi mavuguvugu na mashirika ya Kimataifa ya Wiki ya Mapambano dhidi ya Ubeberu, tunajidhatiti katika mapambano ya kimapinduzi dhidi ya mfumo dume, ukoloni, na ubeberu katika pembe zote za ulimwengu.

Tukiongozwa na mapambano dhidi ya ufashisti na mapambano ya wavujajasho wanawake, Kimataifa Siku ya Wanawake imekuwa alama muhimu kwa mashirika yetu ya kimapinduzi na mavuguvugu kote ulimwenguni kuungana katika vita vya kimataifa dhidi ya mfumo dume, ubepari, na ubeberu.

Sisi wanawake tumeongoza mapambano ya ukombozi ya yaliyokuwa makoloni, kukomesha utumwa, kupinduliwa kwa falme, na kuushinda ufashisti, lakini bado tunaendelea kukabiliwa na ukandamizaji wa kijinsia, kutengwa, na kufanyiwa vurugu mikononi mwa dola na mfumo wa kibepari, na vile vile majumbani, hivyo siku ya Kimataifa ya Wanawake inabaki kuwa wito wa haraka wa kuendeleza mapambano ya ufeministi hadi wote watakapokuwa huru kutoka kwenye ubeberu wa mfumo dume na dola kandamizi.

Machi 8, 2021, inatukumbusha mwaka wa kukithiri kwa majanga ambayo hayajawahi kutokea, kuongezeka kwa madhila ya kibeberu kwa watu katika mapambano kote ulimwenguni, na kuongezeka kwa kasi kwa makundi ya mrengo wa kulia. Wanawake wamekuwa wakibeba mzigo wa majanga haya, na tumepata ongezeko kubwa la ukatili katika ngazi zote.

Pamoja na wanawake kufungamanishwa na umaskini ulimwenguni, sisi ndio wa kwanza kuteseka kutokana na migogoro ya kiuchumi, idadi kubwa ya wenzetu wamefukuzwa kazi, na wengine wengi wanajikimu kwa kazi zisizo rasmi ili kukidhi mahitaji ya kimaisha. Tunakabiliwa na unyonyaji mara tatu zaidi chini ya mfumo wa kibepari wakati huo huo tukipigania ujira, katika hali nyingi tumejitolea katika uangalizi wa nyumba, kazi ya uangalizi wa nyumba imezidi na kuongezeka sana kwa sasa kutokana na hali ya karantini na kufungwa kwa shughuli za mbalimbali za kiuchumi (lockdown).

Wakati nchi za kibepari zinaharakisha kuokoa uchumi wao, wamewaacha wafanyakazi wanaotoa mahitaji ya msingi ya maisha ya mwanadamu kuhatarisha maisha yao katika mstari wa mbele. Wanawake ni kundi kubwa la wale wanaofanya kazi katika tasnia kama uuguzi, utunzaji wa watoto, wazee, lishe, elimu na sisi ndio kundi la kwanza lililo hatarini tunapoendelea kufanya kazi katika mazingira ya sasa ya janga, kudumisha ubinadamu na kuwatunza mamilioni ambao wameugua.

Licha ya ongezeko kubwa la kazi za ndani na kazi ya uangalizi, zote zikiwa ni muhimu kwa ustawi wa maisha, bado wanawake hawaonekani katika muktadha wa mahusiano

ya mfumo dume na mkakati wa kibepari wa kuficha uhusiano wa kiuchumi uliopo kati ya uzalishaji na uzazi.

Wakati huo huo, katika hali ya kufungwa kwa shughuli (lockdown) na mgogoro wa kiuchumi, ukatili dhidi ya wanawake umeongezeka na kufikia viwango vya juu zaidi, kuongezeka kwa mazuio ya mavuguvugu na kufungwa kwa taasisi za kijamii katika nchi za kibepari kumetupa chaguzi chache kuliko hapo awali wale tunaokabiliwa na unyanyasaji wa kisaikolojia, kimwili na ubakaji majumbani.

Tunaendelea kupigania uhuru juu ya miili yetu, majumbani, dhidi ya serikali, katika huduma za afya, na mahali pa kazi, haswa wakati huu ambapo makundi ya mrengo wa kulia yameongezeka na kuuimarisha zaidi udhibiti wa mfumo dume juu ya miili ya wanawake wakati wa shida na janga lililopo.

Katikati ya majanga ya ulimwengu, Ubeberu wa Marekani na washirika wake umeonesha kutokujali kunusuru maisha ya walio wengi ulimwenguni na hata ndani ya mipaka yao wenyewe. Wakati vita baridi, vikwazo, na shughuli za kijeshi zikiongezeka, sisi ndio wa kwanza kukabiliwa na uhaba wa chakula, maji, na dawa, vita vya silaha, na kuhama hama katika makazi yetu. Wakati uvamizi wa kibeberu katika maeneo na uhuru wa nchi vikiongezeka, dada zetu wanalazimishwa kuingia ndani ya jela za kibeberu ambapo wanapata vizuizi vya muda mrefu na kudhalilishwa kama wafungwa wa kisiasa. Wakati mipaka ikifungwa na janga likienea, sisi ambao ni wahamiaji na wakimbizi tunakabiliana na janga kwa kutokuwa na uhakika wa maisha na hatari kwenye kila hatua. Wakati ufashisti na makundi ya mrengo wa kulia yakijiimarisha, tunakabiliwa na ukandamizaji wa haki za kijamii na kisiasa tulizozipigania na kushinda kwa bidii kwa miongo mingi ya mapambano ya wanawake.

Hata hivyo, ni sisi wanawake masikini, weusi, wazawa, wahamiaji, na wanawake wavujajasho tunaoongoza na kupambana katika mstari wa mbele dhidi ya ubeberu. Vikosi vyetu vya mapambano vinaendelea kuongezeka, na mapambano ya wanawake wanamapinduzi na wavujajasho tumeendelea kujenga mavuguvugu yetu na mashirika yetu, tumepata ushindi mwingi licha ya giza la miezi kadhaa iliyopita. Kuanzia wanawake wanamapinduzi wanaoongoza uhamasishaji dhidi ya vurugu za makundi ya mrengo wa kulia, mpaka kwa dada zetu thabiti wanaopigania ukombozi wa Palestina na Sahara Magharibi dhidi ya vikosi vya Kizayuni na vya kibeberu, majasiri wa Cuba, China, Venezuela, na mataifa ya kijamaa yanayotoa misaada na matibabu kwa wanaodhulumiwa, mpaka wanawake wapiganaji wanaoongoza mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi dhidi ya vurugu za polisi na majeshi ulimwenguni, tunaimarishwa na mapambano ya wanawake wanamapinduzi wanaoongoza njia kwa siku za usoni.

**Mapambano dhidi ya ubeberu, dhidi ya ubaguzi wa rangi, ukoloni, na ubepari, hayawezi kupiganwa bila mapambano dhidi ya mfumo dume na bila ushiriki kamili na uongozi wa wanawake!**

**Wanawake Wavujajasho Ulimwenguni, Unganeni!**